# UTANGULIZI

Kuna wakati unakutana na matatizo ambayo huwezi kuyabeba. Unahangaika kufanya hili na lile ili walau ujikwamue, badala ya kujikwamua unakuta unaongeza matatizo zaidi.

Kuna wakati ambapo unahitaji kuweka siraha zote chini na kushikilia pumzi yako tu. Huhitaji kusogea mbele wala kurudi nyuma bali kutulia ulipo na kushikilia pumzi yako. Watu wengi wanaharibikiwa na kuongeza matatizo kutokana na hamaki ya kupatwa na tatizo. Badala ya kutatua tatizo lililotokea wanajikuta wanaongeza tatizo kubwa zaidi.

Wapo watu waliopoteza maisha kwa sababu ya kupewa taarifa ya msiba wa mtu wampendae. Kuna watu wamepoteza ajira kwa sababu ya jinsi walivyopokea manyanyaso na hali ya uonevu kazini.

Wapo pia waliopata ajali kubwa baada ya kupata ajali ndogo na kujaribu kuikimbia ajali hiyo.

Binadamu tumeumbwa kuhamaki tatizo kubwa likitokea na kuhangaika kutafuta majibu ya haraka ili kulitatua. Watu wengi wamejikuta wanaingia kwenye kesi za mauaji kwa sababu tu ya kushindwa kutulia wakati dunia imewaegemea.

Kitabu hiki ni mwongozo wa jinsi mtu yeyote anaweza kupita katika magumu yanayomkabili na kupata mafunzo kutokana na changamoto ile bila kuongeza matatizo zaidi.